

T The Tanganyika Law Society

The Bar Association of Tanzania Mainland

TAARIFA KWA UMMA

Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili cha Tanganyika (Tanzania Bara) (Tanganyika Law Society (TLS)) linapenda kuutarifu umma kuwa uamuzi wa kumuondoa katika Rejista ya Mawakili wa Tanzania Bara, Wakili Fatma Karume, umetolewa leo tarehe 23 Septemba 2020 na Kamati ya Mawakili (**Advocates Committee**) kwa mamlaka yake chini ya Sheria ya Mawakili (**Advocates Act Cap 141 R.E. 2002**) na si Kamati ya Maadili ya Chama cha Mawakili cha Tanganyika (Tanzania Bara) (**The Ethics Committee of Tanganyika Law Society**).

Kamati hizo zina mamlaka tofauti na zimeanzishwa kwa sheria na mamlaka tofauti. Kamati ya Mawakili imeanzishwa na Sheria ya Mawakili (**Advocates Act Cap 141 R.E. 2002**) wakati Kamati ya Maadili ya Chama cha Mawakili Tanganyika (**The Ethics Committee of Tanganyika Law Society**) imeanzishwa na Baraza la Uongozi la TLS kwa mamlaka yake ya kuanzisha kamati zake chini ya Sheria ya Tanganyika Law Society, Sura Namba 307 ya Sheria za Tanzania.

Hivyo ni makosa makubwa kuwahusisha wajumbe wa Kamati ya Maadili ya TLS na uamuzi huo na kusambaza majina yao katika mitandao ya kijamii.

Imetolewa Jijini Dar es Salaam leo tarehe 23 Septemba 2020.



Dkt. Rugemeleza A.K. Nshala
RAISI